Stanbic Bank

MAELEZO NA MASHARTI YA AKAUNTI YA AKIBA YA MUDA MAALUM

Mkataba ulioainishwa hapa chini unaanza kutumika kati yako na Benki wakati wa kuomba Akaunti ya Akiba ya Muda Maalum:

1. **Upatikanaji:** Amana za muda maalum zinapatikana kwa vipindi tofauti vilivyoainishwa nyuma ya fomu. Unatakiwa kuchagua chaguo muafaka na kufuata kikamilifu muda ulioainishwa. Fedha zinapatikana tu baada ya ukomavu wa amana ya muda maalum.

2. **Kiwango:** Benki inaweza kuweka kiwango cha chini au cha juu kwa kila akaunti ya akiba ya muda maalum ambacho sharti kidumishwe na wewe katika kipindi chote kilichoainishwa cha amana.

3. **Fedha za Ziada:** Nyongeza au fedha za ziada zitafunguliwa kama amana ya muda maalum mpya.

4. **Ukomavu.**

   (i) Amana ya muda maalum itakomaa kwenye tarehe inayohusika ya kufunguliwa kwa akaunti na Benki. Ikiwa tarehe hiyo inaangukia kwenye sikukuu ya umma au tarehe nyingine ambayo kwa kawaida Benki haitakuwa wazi kwa biashara, basi uadhimishaji utakuwa katika siku ya kazi inayofuatia

   (ii) Utatakiwa kuishauri Benki kwa maandishi (katika tawi) lako la makazi) kuhusu maelekezo muhimu yoyote ambayo unataka yafanyike wakati wa ukomavu wa akaunti japo siku tatu kabla ya ukomavu wa amana ya muda maalum.

   (iii) Ikiwa unataka amana ya muda maalum iendelee, sharti ujaze fomu ya maombi upya ya akaunti ya amana ya muda maalum.

5. **Riba:** Kiwango cha riba kitapangwa wakati wa ufunguaji wa akaunti ya amana ya muda maalum na kitakokotolewa kwenye kiasi cha amana kuu. Isipokuwa kama itashauriwa vinginevyo, riba haitaongezwa. Riba italipwa tu siku ya ukomavu wa amana ya muda maalum au katika nyakati kama itakavyokubaliwa na Benki katika kipindi cha amana ya muda maalum, baada ya wewe kwanza kuitaarifu Benki kuhusu mahitaji hayo.

6. **Ukombozi wa Mapema**

   (i) Katika mazingira maalum, Benki inaweza kuruhusu ukamilishaji mapema wa amana ya muda maalum, ikiwa utaipatia Benki siku thelathini (30) za taarifa ya maandishi.

Classified as Internal use only

(ii) Ikiwa mapendekezo yako yataidhinishwa na Benki, sharti usamehe riba ya jumla kwenye akaunti ya amana ya muda maalum kwenye Benki, pamoja na kuilipa benki tozo za utoaji zinazohusika.

(iii) Benki pia itarejesha riba yoyote ambayo inaweza kuwa imelipwa maalum na /au kwa vipindi kabla ya ukomo wa amana ya muda maalum kwa kukata viwango hivyo kutoka amana kuu.

7. **Malipo:** Malipo yote, (iwe ya mtaji au riba) yataingizwa moja kwa moja katika Akaunti yako na Benki. Malipo yoyote yatakayofanywa kwenye benki nyingine yoyote kama itakavyoelekezwa na wewe kwa maandishi yatahitaji tozo za ziada.

8. **Jumla:**

i. Utaipata Benki taarifa zote za ziada kama itakavyoombwa na Benki kwa madhumuni ya akaunti ya akiba ya muda maalum kadiri Benki itakavyoona ni lazima.

ii. Benki kwa busara yake, itakuwa na haki ya kubadilisha maelezo na masharti yoyote mara kwa mara kwa kutoa taarifa ya maandishi ya siku thelathini (30) kwako.

iii. Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zitatumika kwenye maelezo na masharti haya.

KWA NA KWA NIABA YA MTU BINAFSI AU WENYE AKAUNTI PAMOJA (futa au ongeza kadiri inavyofaa).

Jina: **Jina:**

_____ _____

Saini na tarehe: **Saini na tarehe:**

_____ _____

Classified as Internal use only